JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE

04 HISABATI

Muda: Saa 1: 30 **Mwaka: 2020.**


Maelekezo


1. Mtihani huu una jumla ya maswali **matano (5)**
2. Jibu maswali **yote**

Katika swali la 1 – 5, kokotoa swali ulilopewa na kisha andika jibu sahihi kwenye nafasi iliyotolewa.

Na.		Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
1.	(a)	Andika namba 12, 659 kwa maneno.		
	(b)	Andika elfu kumi na moja mia moja kumi na moja kwa numerali..		
	(c)	Andika sehemu tatu ya nne katika tarakimu		
	(d)	Andika sehemu iliyotiwa kivuli katika umbo lifuatalo: 		
	(e)	Musa ana miaka 40. Andika umri wa Musa kwa kutumia numerali za kirumi.		
2.	(a)	Panga namba zifuatazo kwa mpangilio unaoanza na namba kubwa hadi ndogo Zaidi: 125, 78, 111, 89, 305, 32, 120.		
	(b)	Andika nmaba inayokosekana katika mfululizo ufuatao: 36, 33, 30 _____, 24.		
	(c)	Andika namba mbili zinazofuatana katika mpangilio ufuatao: X, XV, XX, XXV, _____, _____		
	(d)	Miti minne inatofautiana urefu kwa mpangilio ufuatao: m 5, m 8, m 11, m 14. Je, urefu wa mti wa tano utakuwa kiasi gani iwapo unafuata mpangilo huu?		

Na.		Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
	(e)	Agnes alihesabu namba kwa kupunguza kumi ili kupata namba inayofuata. Iwapo namba ya kwanza ilikuwa 80, tafuta namba ya sita.		
3.	(a)	Zidisha: 282 x 17		
	(b)	Baba alimpa Juma sarafu 10 za shilingi mia tano kila moja. Je, Juma alipewa kiasi gani cha pesa?		
	(c)	Toa; sh. 2, 750 – sh. 120 =		
	(d)	Janeti alinunua vitu vifuatavyo sokoni: Machungwa 6 kila mja sh. 200, daftari moja kw ash. 2,000 na kalamu 3 kila moja sh. 700. Je, jumla alilipa shilingi ngapi?		
	(e)	Jumlisha; Saa dakika 5 38 + 3 45		
4.	(a)	Umbo lenye pande nne zinazolingana urefu huitwa _____		
	(b)	Nusu lita 10 za maji ni sawa na lita ngapi za maji?		
	(c)	Badili gramu 16,000 kuwa kilogramu.		

Na.		Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
	(d)	Bustani ya shule ina urefu wa m 25. Je, urefu huo ni sawa na sentimeta ngapi?		
	(e)	Shule ya msingi Chatanda iko umbali wa km 2 kutoka barabara kuu. Je, shule hiyo ipo umbali wa meta ngapi kutoka barabara kuu?		
5.	(a)	Anold alifanya jaribio la Hisabati katika siku tatu za wiki, yaani Jumatatu, Jumatano na Ijumaa. Alama alizopata zimeonyeshwa kwenye grafu ya mhimili ufuatao:		
		 Je ni siku gani alipata alama za juu Zaidi?		
	(b)	Jedwali lifuatalo linaonesha idadi ya wanafunzi wa darasa la tatu waliofaulu mtihani wa mwezi katiika shule ya msingi Kazamwendo. **Mwezi** / **Idadi ya Wanafunzi** Februari 68 Machi 74 Aprili 52 Mei 69 Je, ni mwezi gani wanafunzi wengi Zaidi walifaulu mtihani wa mwezi?		

Na.		Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
	(c)	Wastani wa mauzo ya kalamu katika duka la Kapeto kwa siku nne yameoneshwa katika jedwali lifuatalo: **Siku** | **Mauzo** Jumatatu | Sh. 22,000 Jumanne | Sh. 21,000 Jumatano | Sh. 23,000 Alhamisi | Sh. 20,000 Mauzo madogo kuliko yote yalikuwa ni shilingi ngapi?		
	(d)	Idadi ya vitabu vya kusoma vilivyotolewa na serikali kwa miaka minne katika shule moja ni kama ifuatavyo: Mwaka | Idadi 2002 | 132 2003 | 135 2004 | 142 2005 | 124		
	(e)	Tani za mpunga zilizovunwa kwenye shamba la mkulima ziliongezeka sawia kila mwaka kwa miaka minne mfululizo na tani hizo zilionyeshwa kwenye grafu ya mhimili ufuatao:  Je, jumla ya tani ngapi zilivunwa kwa miaka yote minne?		